

## 2. Zipo Idara zifuatazo.

- Idara ya Uongozi
- Idara ya Mipango
- Idara ya Ufundu
- Idara ya Uhusiano
- Idara ya Audiovisual

Radio Sauti ya injili si ya Kibashara, hii ni Radio ya Kanisa hivyo kwa maadili yake haifanyi biashara, inatoa huduma kwa jammii nzima,pamoja na huduma hizo tunapokea matangazo mbali mbali, ya biashara, dini , vifo, harus, kupotea mtu na vitu, kwa bei nafuu sana.Waweza kuchangia kituo hiki kwa huduma ya M-pesa kwa namba zifuatazo.  
**0758 922 922 au 0655922922**  
unaweza kulipia tangazo lako kwa namba hizo.



### SIKILIZA VIPINDI MBALIMBALI KAMA


AFYA NI UHAI  
HABA NA HABA  
KILIMO NI UTAFITI  
FAHAMU HAKI ZAKO  
DIRA YA LEO  
MAFUNDISHO YA MWL. MWAKASEGE  
WAZEE NI HAZINA  
SAA YA IMANI  
KWELI ITAKUWEKA HURU  
CHUNGA KONDOO ZANGU  
MAZINGIRA YETU  
WANAWAKE WA MATUMAINI  
SAA YA WATOTO  
VIJANA MASHULENI  
HARAKATI ZA VIJANA  
TUMWABUDU MUNGU WETU  
TATIZO LANGU  
KRISTO KWA MATAIFA YOTE  
UKIMWI NA MAISHA



### Kwa mawasiliano na Radio Sauti ya Injili.

S.L.P 777 Moshi Tanzania  
E-mail-[redio@elct.org](mailto:redio@elct.org)  
Website [www.sautiyainjili.org](http://www.sautiyainjili.org)  
simu namba +2552727 52772,  
+2552727 53080

### KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA (KKKT)



### RADIO SAUTI YA INJILI MOSHI TANZANIA

#### MASAFA YA FM

92.3 MOSHI  
96.3 ROMBO  
100.3 SAME  
96.1 ARUSHA  
102.6 USAMBARA  
96.5 TANGA  
102.9 KIBAYA  
99.9 MOROGORO  
102.9 MONDULI

[redio@elct.org](mailto:redio@elct.org)

[www.sautiyainjili.org](http://www.sautiyainjili.org)

## **HISTORIA YA RADIO SAUTI YA INJILI MOSHI -TANZANIA**

Radio Sauti ya Injili Moshi , ni Radio pekee ya binafsi tangu uhuru wa Tanzania bara mwaka 1961 ikihusika zaidi na kutangaza vipindi vyta dini na vya kimaendeleo kwa jamii.Lengo kuu la Radio Sauti ya injili tangu kuanzishwa kwake mwaka 1963 ni kumtangaza kristo katika ulimwengu wote.Ikitangaza siyo Tanzania tu bali Afrika Mashariki, Kati,Kusini na Mashariki ya mbali. Vipindi vyta Redio hii viliandaliwa hapa Moshi na kutumwa masafa mafupi (SW) Addis Ababa Ethiopia. Lakini serikali ya Mfalma Haile Sellasie ilipinduliwa mwaka 1974 na kituo cha Radio Sauti ya injili Addis Ababa kilitafishwa mwaka 1977 na hivyo kusababisha Radio Sauti ya Injili Moshi kupeleka vipindi vyake FEBA radio Ushelisheli

Mitambo hiyo haikuwa na nguvu ya kutosha.



Kwa ajili hiyo tangu mwaka 1979 Radio Sauti ya injili imekuwa ikipel-eka vipindi vyake "Trans world Radio" Manzini Swaziland kwa njia ya posta. Vipindi vyta mwezi mzima viliandaliwa na watumishi wa Redio hii na kusafirishwa ili virushwe hewani vikiwa vimehifadhiwa kwenye reel.



MKU-

RUGENZI WA RADIO SAUTI YA INJILI  
BW. PHILEMON MARK FHAVANGO

Kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia tulihama kutoka kurekodi vipindi kwenye real kwenda kwenye cassette na baadae kwenye Cd, na vilikuwa vinarushwa kwa dakika 30 asubuhi na dakika 45 usiku. Hadi mwezi Julai mwaka 2009 tulisitisha matangazo hayo kutokana na gharama za kurusha vipindi kupanda.

Kuanzia Novemba 27 mwaka 1994 Radio Sauti ya Injili ilianzisha masafa ya FM na kuwa chombo muhimu mno kinachopenya na kuwafikia watu wengi wa mataifa yote na hali zote kirahisi. Tulianza kutangaza kwa majaribio kwa muda wa saa 6 (sita) na baadae saa 18 kwa siku na kuanzia Oktoba 15 mwaka 2010 tupo hewani kwa saa 24.

### **PICHA YA WATUMISHI**



### **HUDUMA ZITOLEWAZO NA RADIO SAUTI YA INJILI**

1.Ina watumishi wataalam wa fani ya utangazaji, uandishi na uandaaji wa vipindi wenyewe ujuzi mkubwa wa muda mrefu, ikiwa ni pamoja na mafundi mitambo.Baadhi yao wanaweza kuendelezwa zaidi.